**HOTUBA YA MHESHIMIWA JOEL ARTHUR NANAUKA (MB), WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS – MAENDELEO YA VIJANA KATIKA UFUNGUZI WA VIJANA PLATFORM KWA VIJANA WA VYUO VIKUU NA VYA KATI MKOA WA TABORA**

---

- **Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa wa Tabora;**
- **Katibu Tawala wa Mkoa;**
- **Viongozi wa Vyuo Vikuu na Vyuo vya Kati;**
- **Wawakilishi wa Taasisi za Umma na Binafsi;**
- **Viongozi wa Taasisi za Fedha;**
- **Wadau wa Maendeleo ya Vijana;**
- **Ndugu vijana;**
- **Waandishi wa Habari;**
- **Mabibi na Mabwana.**

**Kazi na Utu, …**

**Vijana tuyajenge…**

Awali ya yote, ninapenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia afya njema na kutukutanisha leo hapa Mkoa wa Tabora katika tukio muhimu la ufunguzi wa Vijana Platform kwa vijana wa Vyuo. Pia, ninapongeza Uongozi wa Mkoa wa Tabora chini ya Mheshimiwa Paul Chacha na timu yake yote inayomsaidia katika kutekeleza majukumu ya Serikali. Hongereni sana kwa kuendelea kumsaidia Dkt. Samia Suluhu Hassani Rais wa Jamhuri ya

Muungano wa Tanzania katika kuleta Maendeleo ya Taifa letu. Kama mnavyofahamu Mkoa wa Tabora ni kitovu cha historia, biashara na kilimo, na una nafasi kubwa ya kukuza vipaji na ubunifu wa vijana.

**Ndugu vijana,**

Vijana Platform ni jukwaa la kitaifa lililozinduliwa tarehe 10 Januari 2026 jijini Dar es Salaam. Lengo lake ni kuunganisha vijana na Serikali yao ili kuimarisha ushiriki wao katika maamuzi, kuwapatia taarifa za fursa za ajira na ujasiriamali, na kujenga kizazi chenye uzalendo na uwajibikaji. Baada ya uzinduzi huo majukwaa ya aina hiyo yamefanyika katika Mkoa wa Singida (Campus-Connect), Mwanza, Shinyanga na leo hii linafanyika hapa katika Mkoa wa Tabora kwa kuwalenga Vijana waliopo Vyuoni.

Kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi 2022 (PHC 2022), vijana wa miaka 15–35 ni takribani milioni 20.6, sawa na asilimia 34.4 ya Watanzania wote. Hii ni rasilimali kubwa ya Taifa. Serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi wa Mheshimiwa Samia Suluhu Hassani imeweka msisitizo mahsusi katika kuwawezesha vijana kiuchumi na kijamii.

Tunatambua dhamira yake ya dhati katika kuwawezesha na kuwaendeleza vijana na ndiyo maana akaunda Wizara mahsusi ya Maendeleo ya Vijana na kuiweka chini ya Ofisi yake na akaniteua niweze kuwatumikia vijana wa Tanzania.

Ninapenda kuwafahamisha kuwa, kupitia Ofisi ya Rais – Maendeleo ya Vijana, tunaongozwa na falsafa ya:

1. Kufanya kazi kwa kasi;
2. Viongozi kufikika;
3. Matumizi ya teknolojia kuwafikia vijana wengi zaidi.

Aidha, Serikali imetenga shilingi bilioni 200 kwa ajili ya uwezeshaji wa kiuchumi kwa vijana kupitia sekta mbalimbali. Lengo ni kuhakikisha vijana wanapata mitaji, mafunzo na mazingira rafiki ya kuanzisha na kukuza biashara.

**Ndugu vijana,**

Kama nilivyodokeza hapo mwanzo, Mkoa wa Tabora una fursa nyingi ambazo, endapo tutazitumia vizuri tutakuwa tumepunguza sana changamoto ya ukosefu wa ajira. Vijana mnaweza mkashiriki katika kilimo cha mazao ya biashara na mazao ya chakula, biashara ndogo, uchimbaji mdogo wa madini, pamoja na sekta ya huduma. Kupitia jukwaa hili, tunataka kufungua ndoto zenu, ili muanze mapema mkiwa Vyuoni kuweka malengo mahsusi ya kufikia ndoto zenu, muandae mawazo ya biashara ambayo yataongeza thamani katika mnyororo wa uzalishaji, na kuzalisha ajira kwa vijana wengine.

Kupitia Vijana Platform (Compus Connect), Vijana mtasikilizwa na mtatoa maoni yenu kuhusu Changamoto mnazokabiliana nazo ili kuzitafutia ufumbuzi kwa pamoja kwa kushirikiana na Serikali. Pia, mtaunganishwa na fursa zilizopo ambazo zinatolewa na Taasisi za fedha na Wadau wengine wa Maendeleo.

Vilevile, tutaibua vipaji, uthubutu na ubunifu wenu vijana ili uweze kutumika katika kuleta maendeleo yenu na Taifa kwa ujumla. Ni muhimu kutambua kuwa jukwaa hili ni la ushiriki mpana wa vijana wote bila ubaguzi.

**Ndugu vijana,**

Ninawahimiza mtumie fursa hii kikamilifu, anzeni kujiandaa mapema huku mkijua kuna maisha mengine baada ya Chuo ambapo mtakuwa mnategemewa na Jamii. Elimu tunayoipata hapa itusaidie katika kukabiliana na changamoto zinazoikabili jamii na kupata suluhisho. Jiungeni, toeni mawazo, anzisheni miradi, na shirikianeni kujenga Tabora na Tanzania ya kesho. Serikali ipo pamoja nanyi, na mustakabali wa Taifa letu uko mikononi mwenu. Kupitia Jukwaa hili, pia nimeombwa kutoa zawadi ya fedha kama mtaji kwa Vijana Watano walioibuka washindi wa Mawazo bora ya biashara ili waanze kuyatekeleza wakiwa Chuoni, kazi hiyo nitaifanya hapo baadaye.

Kabla ya kuhitimisha, ninatoa rai kwa Wanafunzi wa Vyuo vyote vya Mkoa wa Tabora kutafuta na kutumia fursa zilizopo ili pindi mnapohitimu masomo yenu, msihangaike kutafuta kuajiriwa bali kuwa watengeneza ajira. Leo hii nimetaarifiwa kuwa wapo wataalamu watakaotoa mada kuhusu fursa mbalimbali. Pia, tutapata kusikia shuhuda za Vijana wenzenu walioona fursa wakazitumia na wamefanikiwa kwa kuboresha maisha yao.

Mwisho, lakini siyo kwa umuhimu, ninawashukuru viongozi wa Mkoa wa Tabora, Vyuo vyote vilivyoshiriki, na Wadau wote waliofanikisha tukio hili. Serikali inatambua mchango wenu.

Baada ya kusema hayo, sasa natamka rasmi kuwa Vijana Platform kwa vijana wa Vyuo Vikuu na Vyuo vya Kati (Compus Connect) katika Mkoa wa Tabora limefunguliwa ili tuweze kuendelea na mjadala.

**Asanteni sana kwa kunisikiliza.**

**Mungu ibariki Tanzania.**

**Mungu awabariki vijana wa Tanzania.**